## OFISI YA RAIS

# UTUMISHI

## NA UTAWALA BORA



Toleo la Julai - Septemba, 2025

# YALIYOMO


1 WAZIRI MKUU MHE. MAJALIWA ATOA WIKI TANO TAASISI ZA SERIKALI KUJIUNGA NA MFUMO UNAOWEZESHA SERIKALI KUWASILIANA 1

2 MHE. SIMBACHAWENE ATEMBELEA JENGO JIPYA LA SEKRETARIETI YA AJIRA, ATOA SHUKRANI KWA RAIS MHE. DKT. SAMIA KWA KUWEZESHA UJENZI NA MAELEKEZO YALIBORESHA MCHAKATO WA AJIRA 4

3 MHE. SIMBACHAWENE AITAKA TAKUKURU IZIDISHE MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA 7

4 IBADA MAALUM YA KUMBUKIZI YA MIAKA MITANO (5) YA KIFO CHA RAIS MSTAAFU WA AWAMU YA TATU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA HAYATI BENJAMIN WILLIAM MKAPA 9

5 NAIBU WAZIRI SANGU APONGEZA WIZARA NA TAASISI ZA UMMA KWA KUWA NA UTAYARI WA KUWAHUDUMIA WATUMISHI WA UMMA NA WANANCHI KATIKA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA 11

6 SEKRETARIETI ZA MIKOA NA WIZARA ZASISITIZWA KUZINGATIA MISINGI NA MIIKO YA UONGOZI 13

7 KATIBU MKUU MKOMI ASISITIZA DHANA YA URITHISHANAJI MADARAKA KWA WATUMISHI WA UMMA NCHINI 16

8 KATIBU MKUU MKOMI ATEMBELEA MABANDA YA WIZARA NA TAASISI ZA UMMA KWENYE WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, ATOA SHUKRANI KWA USHIRIKI 22

9 KAMATI YA KITAIFA YA KUDHIBITI VVU, UKIMWI NA MSY MAHALI PA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA YATAKIWA KUIMARISHA MALENGO YA KUDHIBITI MAGONJWA HAYO 24

10 WATUMISHI OFISI YA RAIS-UTUMISHI WASHIRIKI KONGAMANO LA NNE LA MADEREVA WA SERIKALI WA TANZANIA 26

11 WARATIBU WA JINSIA WATAKIWA KUTOA ELIMU KWA WATUMISHI WA UMMA JUU YA NAMNA YA KUKABILIANA NA VIKWAZO MAHALI PA KAZI 27

12 UTUMISHI YATWAA UBINGWA WA MPIRA WA MIGUU SHIMIWI KWA MARA NYINGINE 29

13 TIMU YA MPIRA WA PETE OFISI YA RAIS - UTUMISHI YAFUZU KUINGIA ROBO FAINALI 30

14 TIMU YA MPIRA WA PETE OFISI YA RAIS - UTUMISHI YAFUZU KUINGIA ROBO FAINALI 31

15 KATIBU MKUU MKOMI APOKEA MAKOMBE YA USHINDI MASHINDANO YA SHIMIWI 2025 ASISITIZA UMUHIMU WA MICHEZO KWA WATUMISHI 32

# 1 WAZIRI MKUU MHE. MAJALIWA ATOA WIKI TANO TAASISI ZA SERIKALI KUJIUNGA NA MFUMO UNAOWEZESHA SERIKALI KUWASILIANA

*Na Mwandishi Wetu - Dodoma*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa ameziagiza Taasisi za Serikali ambazo hazijajiunga na mfumo wa kielektroni utakaowezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana (GovESB) kujiunga na mfumo huo ifikapo Julai 30 mwaka huu ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia katika kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Mhe. Majaliwa ametoa maagizo hayo wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma.

"Taasisi zote za umma ambazo hazijajiunga na mfumo huu mwisho ni Julai 30 mwaka huu, wote mhakikishe mmejiunga GovESB, huu ni msisitizo ambao ulitolewa na Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa kila taasisi ipeleke mfumo wake eGA, idadi ya taasisi zilizounganishwa ni chache, hakuna gharama na hutakiwi kupanga bajeti".

Mhe. Majaliwa ameongeza kuwa mfumo huo unafaida kubwa katika utumishi wa umma kwani utasaidia kurahisisha utendaji, kutoa taarifa kwa wakati, kuondoa makosa ya kibinadamu katika kuwahudumia wananchi pamoja na kuwabana wala rushwa. "Nimefurahi kujulishwa kwamba jumla ya mifumo 223 kutoka kwenye taasisi 185 imeunganishwa na kusomana".

Aidha, Mhe. Majaliwa ametoa wito kwa taasisi zote za umma zenye mifumo na zinazoendelea kubuni mifumo zihakikishe mifumo hiyo inasomana na inaweza kubadilishana taarifa kupitia mfumo huo wa GovESB ikiwa ni njia mojawapo ya kuendelea kuboresha huduma za Serikali.

Kadhalika, Mhe. Majaliwa ameitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kuhakikisha mifumo iliyounganishwa inaendelea kubadilishana taarifa pamoja na kujiridhisha kwa kila anayeingia awe na uwezo wa kuwasiliana na wengine wote waliomo ndani.

Katika hatua nyingine, Mhe. Majaliwa ametoa wito kwa watumishi wa umma kuzingatia miiko na maadili ya utumishi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingitia Sera na Sheria kwa manufaa na maendeleo ya Taifa letu.

"Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana watumishi wote wa umma nchini, niwahikishie kuwa serikali ya awamu ya sita iko pamoja nanyi, fanyeni hivyo kwa ajili ya manufaa na maendeleo ya Taifa letu", amesema Mhe. Majaliwa.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe.George Simbachawene amesema Tanzania imetambulika kimataifa ambapo mwaka 2022 Benki ya Dunia ilifanya utafiti kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia duniani katika utoaji wa huduma za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi.

Amefafanua kuwa ripoti ya utafiti huo iliyotolewa Machi, 2023 ilibanisha kuwa Tanzania imefanikiwa kupanda daraja kutoka kundi B hadi kundi A na kushika nafasi ya 26 duniani, nafasi ya 2 Afrika na nafasi ya kwanza katika nchi za Afrika Mashariki.

Katika tukio hilo, Mhe. Majaliwa amezindua mifumo miwili ambayo ni Mfumo wa kielektroni unaowezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa ujulikanao kama Government Enterprises Service Bus (GovESB) pamoja na Mfumo wa e-Wekeza unaomuwezesha Mtumishi wa Umma kuwekeza katika Mfuko wa Faida (Faida Fund).

Siku ya Utumishi wa Umma husherehekewa Juni 23 kila mwaka na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kwa lengo la kutambua mchango wa Watumishi wa Umma katika maendeleo ya nchi zao na Bara la Afrika kwa ujumla.




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akizindua rasmi Mfumo wa Kubadilishana Taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus-GovESB) katika Kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*



*Baadhi ya Watumishi wa Umma na Wananchi wakisikiliza hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa wakati akimwakilisha Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akiteta jambo na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (kushoto) wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akitazama nyaraka za Kiutumishi alipotembeleea banda la Ofisi ya Rais-UTUMISHI alipomwakilisha Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kilele cha Wiki ya Utumishi wa Umma kwenye viwanja vya Chinangali jijini dodoma.*



*Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakifuatilia hotuba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa wakati akimwakilisha Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*




*Viongozi, Watumishi wa Umma na Wananchi wakiwa katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 yaliyofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma.*




2

# MHE. SIMBACHAWENE ATEMBELEA JENGO JIPYA LA SEKRETARIETI YA AJIRA, ATOA SHUKRANI KWA RAIS MHE. DKT. SAMIA KWA KUWEZESHA UJENZI NA MAELEKEZO YALIBORESHA MCHAKATO WA AJIRA

*Na Veronica Mwafisi - Dodoma*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene ametembelea jengo jipya la Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na kutoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha rasilimali fedha za ujenzi wa jengo hilo na maelekezo ambayo amekuwa akiyatoa mara kwa mara ya kuboresha shughuli za taasisi hiyo ikiwemo mchakato mzima wa ajira nchini.

Akizungumza na Watumishi wa Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma mara baada ya kufika katika Ofisi hiyo iliyopo eneo la Tambukaleri jijini Dodoma, Mhe. Simbachawene amesema mahitaji ni mengi lakini Rais aliona ni muhimu pamoja na mambo mengine suala la ajira likapewa kipaumbele hasa kwa kuwa na jengo lake katika uendeshaji wa mchakato wa ajira.

“Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita hasa Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo mbalimbali na utashi wake binafsi wa kutuwezesha kuwa na jengo hili na majengo mengine yaliyo chini ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, haya yote yasingewezekana kwa sababu mahitaji ni mengi” Mhe. Simbachawene ameongeza.

Mhe. Simbachawene ameipongeza Bodi na Menejimenti ya Ofisi hiyo kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa jengo hilo na wote waliohusika ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuhakikisha jengo la ofisi hiyo linakamilika kwa ustadi.

“Lengo langu leo ni kuangalia jengo, kwa kweli jengo limejengwa kwa ustadi mkubwa sana, niwapongeze wataalam wote waliohusika katika ujenzi na waliosimamia, jengo lina mvuto na thamani ya fedha inaonekana.” Mhe. Simbachawene amesisitiza.

Aidha, Mhe. Simbachawene amezungumzia suala la mchakato wa ajira kufanyika mikoani na kuchukua barua za ajira mikoani kuwa ni maelekezo ya Rais ambayo alielekezwa ili kupunguza gharama na muda wa wasailiwa.

“Maelekezo yote ya kuboresha mchakato wa ajira ambayo nilikuwa nikiyatoa kwa Bodi na Menejimenti nilikuwa nikipewa na Rais, hivyo hatuna budi kumshukuru kwa maelekezo yake yenye kujenga” Ameongeza.

Mhe. Simbachawene amewasisitiza watumishi wa Ofisi hiyo kuendelea kusimamia kikamilifu zoezi la usaili wa ajira na kuwa makini ili wenye sifa wapate ajira kwa haki bila upendeleo.

Naye Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu ameipongeza Sekretarieti ya Ajira kwa kuwa wepesi kupokea maelekezo mbalimbali yaliyokuwa yakitolewa na viongozi ili kuboresha utendaji kazi wa taasisi hiyo.

Amewataka watumishi wa ofisi hiyo kutumia ofisi hiyo mpya kama chagizo la morali ya kufanya kazi.

“pongezi kwa ofisi kuwa na jengo lake na Mhe. Simbachawene kwa maelekezo, usimamizi na uongozi vimeonekana kwa vitendo. Mimi ni shahidi, nimekuwa nikipokea maelezo yako ya kushughulikia changamoto za taasisi hii.” Mhe. Sangu amesema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wajumbe wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bibi Sofia Kaduma amemshuru Waziri Simbachawene kwa miongozo na maelekezo ambayo amekuwa akiyatoa kwa Bodi na Menejimenti hiyo ambayo yameongeza ufanisi na kuleta tija kwa taifa.

Kwa upande wake Katibu wa Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, Bwana Mick Kiliba amesema utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi hiyo ulianza tarehe mwezi Aprili, 2022 kupitia Mshauri Elekezi wa Mradi (Chuo Kikuu cha Ardhi) kupitia Kampuni ya ARU Built Environment Consulting Company Limited (ABECC).




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza na Viongozi na Watumishi ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (hawapo pichani) jijini Dodoma wakati alipotembelea jengo jipya la ofisi hiyo iliyopo eneo la Tambukareli jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (wakwanza kushoto) akisalimiana na Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Bw. Mick Kiliba (wakwanza kulia) wakati Waziri huyo alipotembelea jengo jipya la ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo eneo la Tambukareli jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akifurahia jambo na Viongozi wa ofisi yake na Watendaji wa ofisi ya Sekretarieti ya Ajira wakati wakikagua ukumbi wa kufanyia usaili kwenye jengo jipya la ofisi hiyo iliyopo eneo la Tambukareli jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akisalimiana na baadhi ya watumishi wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma mara baada ya kuwasili katika jengo jipya la ofisi hiyo lililopo eneo la Tambukareli jijini Dodoma.*




*Mwonekano wa Jengo jipya la Sekretarieti ya Ajira lililopo eneo la Tambukareli jijini Dodoma.*



3

# MHE. SIMBACHAWENE AITAKA TAKUKURU IZIDISHE MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

*Na Lusungu Helela - Simiyu*

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene ameitaka Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) kuzidisha mapambano dhidi ya rushwa kubwa huku akisisitiza mapambano dhidi ya rushwa ndogo ndogo yasiachwe kwani ndizo zimekuwa kero kubwa kwa watu wengi hususan watu wa kipato cha chini katika maeneo ya huduma za jamii nchini.

Amesema ni muda muafaka sasa kwa TAKUKURU kuanza kushughulikia rushwa hizo ndogondogo katika maeneo ya masoko, vituovya polisi, shule, zahanati na maeneo mengine ya umma ambako baadhi ya watu wanajulikana na wamejigeuza bila kutoa chochote huwezi kuhudumiwa.

Mhe. Simbachawene ametoa kauli hiyo Mkoani Simiyu wakati akizindua jengo la Ofisi ya TAKUKURU Mkoa ambalo hadi kukamilika kwake limegharimu kiasi cha Sh. milioni 640.

Amesema rushwa za namna hiyo zimekuwa zikiwakera watu wengi wa tabaka la chini ambao ndio wengi hali inayochochea wananchi kuanza kuichukia Serikali.

Amesema wakishughulika na rushwa hizo wananchi watakuwa na furaha na watazidisha imani waliyokuwa nayo kwa Serikali yao.

Amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya rushwa, uwekezaji wake wa fedha, rasilimaliwatu na vitendea kazi ni utashi alionao kwa TAKUKURU ili iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi.

"Rushwa ni adui wa ustawi wa jamii, rushwa inapofusha, TAKUKURU mpo kamateni vinara wa rushwa katika maeneo hayo kwani wanajulikana kwa majina na vyeo vyao " amesisitiza Mhe.Simbachawene.

Kufuatia hatua hiyo, Mhe.Simbachawene ametoa wito kwa viongozi wa dini na wadau wengine kusaidia katika mapambano hayo kwani TAKUKURU pekee haiwezi na hivyo inahitaji ushiriki wa wadau ili kukemea na kuwafichua wale wote ili sheria ichukue mkondo wake.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Bw. Crispin Chalamila amesema Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye ujenzi wa majengo katika wilaya na mikoa mbalimbali nchini na hii ni kuonesha utashi wa Mhe.Rais katika mapambano dhidi ya rushwa nchini.

Amesema katika bajeti ya mwaka 2024/ 2025 kiasi cha shilingi Bilioni mbili zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya TAKUKURU nchini ikiwemo jengo hilo la TAKUKURU Mkoa wa Simiyu.

Chalamila amesema ujenzi wa jengo hilo utachagiza mapambano dhidi ya rushwa ambapo hapo mwanzo jengo walilokuwa wamepanga lilikuwa kwenye makazi ya watu hali iliyopelekea hata wale wananchi wenye taarifa fiche kuogopa kuja ofisini hapo kwa hofu ya kuonwa na watu, " ila kwa ofisi hii naamini wananchi watakuwa huru kutuletea taarifa bila hofu ya kuonwa na yeyote " amesisitiza Chalamila.




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza na baadhi ya wananchi, watumishi na viongozi kutoka Taasisi mbalimbali wakati akizindua Jengo la TAKUKURU Mkoa wa Simiyu ambalo limegharimu kiasi cha Sh. Mil. 640 hadi kukamilika kwake.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akisalimiana na baadhi ya watumishi na viongozi mbalimbali kutoka Taasisi mbalimbali alipowasili kwa ajili ya kuzindua Jengo la TAKUKURU Mkoa wa Simiyu ambalo limegharimu kiasi cha Sh. Mil. 640*



*Baadhi ya wanachi, watumishi na viongozi kutoka Taasisi mbalimbali wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene wakati akizungumza kabla ya kuzindua Jengo la TAKUKURU Mkoa wa Simiyu ambalo limegharimu kiasi cha Sh. Mil.640 hadi kukamilika kwake.*

# 4 IBADA MAALUM YA KUMBUKIZI YA MIAKA MITANO (5) YA KIFO CHA RAIS MSTAAFU WA AWAMU YA TATU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA HAYATI BENJAMIN WILLIAM MKAPA




*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (watatu kutoka kulia) akifuatilia Ibada maalum ya kumbukizi ya miaka mitano (5) ya kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Kijiji cha Lupaso Mkoani Mtwara. Wengine ni viongozi mbalimbali walioshiriki Ibada hiyo.*

*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akiwasili nyumbani kwa aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa kijijini Lupaso wakati wa Ibada maalum ya kumbukizi ya miaka mitano (5) ya kifo cha Rais huyo iliyofanyika kijijini hapo. Kushoto kwake ni Katibu Mkuu wa ofisi hiyo Bw. Juma Mkomi.*






*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (watatu kutoka kulia) akifuatilia Ibada maalum ya kumbukizi ya miaka mitano (5) ya kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Kijiji cha Lupaso Mkoani Mtwara. Wengine ni viongozi mbalimbali walioshiriki Ibada hiyo.*




*Sehemu ya Wakurugenzi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Utawala Bora wakiwa Ibada maalum ya kumbukizi ya miaka mitano (5) ya kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Kijiji cha Lupaso Mkoani Mtwara.*




*Wananchi wakiwa katika Ibada maalaum ya kumbukizi ya miaka mitano (5) ya kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa iliyofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Kijiji cha Lupaso Mkoani Mtwara.*

# 5 NAIBU WAZIRI SANGU APONGEZA WIZARA NA TAASISI ZA UMMA KWA KUWA NA UTAYARI WA KUWAHUDUMIA WATUMISHI WA UMMA NA WANANCHI KATIKA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

*Na Veronica Mwafisi - Dodoma*

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu ametoa pongezi kwa Wizara na Taasisi za Umma kwa kuwa na utayari wa kuwahudumia watumishi wa umma na wananchi katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayoendelea katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.

"Tumekuwa tukifanya kliniki katika mikoa mbalimbali kwa ajili ya kutatua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili Watumishi wa Umma na Wananchi, lakini kupitia Maadhimisho haya ya Wiki ya Utumishi wa Umma yamekuwa suluhisho kwa kufanya kazi papo kwa hapo kwani Watumishi wa Umma na Wananchi wamekuja kuhudumiwa kwa wakati,hii inaonesha ni kwa namna gani mmekuwa na utayari wa kutoa huduma bora kwa maslahi ya taifa, hongereni sana," Mhe. Sangu amesema

Aidha, Mhe. Sangu ametoa rai kwa Watanzania wote kufika katika Viwanja hivyo ili kupata huduma za moja kwa moja na elimu kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara na taasisi za Umma.

Katika hatua nyingine, Mhe. Sangu amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali watumishi wa umma nchini kwa kuboresha maeneo yao ya kazi kwa kuwa sehemu salama ili watanzania waweze kupata huduma bora.




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu (kushoto) akisalimiana na Katibu Mkuu wa ofisi hiyo Bw. Juma Mkomi (kulia) baada ya Naibu Waziri huyo kuwasili katika Viwanja vya Chinangali Park kutembelea mabanda ya Wizara na Taasisi zilizoshiriki Wiki ya Utumishi wa Umma jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu (aliyekaa kushoto) akifurahia kucheza mchezo wa drafti wakati alipotembelea banda la Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Viwanja vya Chinangali Park kwenye Wiki ya Utumishi wa Umma jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu (aliyenyoosha mkono) akisisitiza jambo alipotembelea banda la Wizara ya Ujenzi kwenye Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu (kulia) akizungumza na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi-Zanzibar walipokuwa wakijitambulisha baada ya kutembelea Viwanja vya Chinangali Park Jijini Dodoma kwemye Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025.*

# 6 SEKRETARIETI ZA MIKOA NA WIZARA ZASISITIZWA KUZINGATIA MISINGI NA MIIKO YA UONGOZI



*Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi akiwa katika picha ya pamoja na Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Wizara mara baada ya kufungua mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Viongozi hao kwenye mabadiliko ya kifikra, kitabia na mtazamo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kiutumishi yaliyofanyika Mtumba katika ukumbi wa Jiji Dodoma.*

*Na. Eric Amani - Dodoma*

Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Xavier Daudi ametoa wito kwa Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Wizara kuzingatia misingi na miiko ya Uongozi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi na Watumishi wa Umma.

Bw. Daudi ametoa wito huo wakati akifungua mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Viongozi hao kwenye mabadiliko ya kifikra, kitabia na mtazamo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Serikali kwenye mafunzo yaliyofanyika Ukumbi wa Jiji Dodoma.

Kaimu Katibu Mkuu Daudi amesema, Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kuwajengea uwezo wa kiutendaji viongozi lakini Ofisi ya Rais-UTUMISHI imeendelea kupokea malalamiko yanayokwamisha utendaji mzuri wa taasisi za umma jambo ambalo linasababishwa na kutozingatia misingi na miiko ya uongozi.

"Pamoja na serikali kufanya jitihada kubwa ya kuwajengea uwezo viongozi kiutendaji, bado ofisi yetu imekuwa ikipokea malalamiko mbalimbali ikiwemo uwepo wa makundi katika ofisi, kukosa utendaji wa pamoja, upendeleo katika kutoa huduma kwa wadau, kutowaendeleza watumishi, kutotenga bajeti kwa ajili ya kuandaa mipango ya mafunzo inayozingatia mahitaji ya Watumishi itakayoleta manufaa katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi," ameongeza Bw. Daudi.

Aidha, Bw. Daudi amewasisitiza Viongozi hao kuwajengea uwezo wa kiuongozi watumishi walio chini yao ili kuwa na mpango wa urithishanaji madaraka pindi kiongozi anapoondoka katika ofisi awepo mtu mahiri kutoka katika ofisi hiyo wa kushika nafasi hiyo.

Amesema masuala yote hayo yasipotekelezwa yanaenda kinyume na maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akisisitiza misingi ya utawala bora na maadili katika utumishi wa umma.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Idara ya Uendelezaji Rasilimaliwatu Ofisi ya Rais – UTUMISHI, Bi. Leila Mavika amesema Idara anayoiongoza imekuwa ikitoa mafunzo kwa Viongozi na watumishi wa umma ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha.

"Mafunzo ni suala endelevu, hivyo viongozi na watumishi wanapaswa kuendelezwa kwa kujengewa uwezo katika maeneo mbalimbali ili wafahamu namna ya kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia uongozi bora, maadili, akili hisia na kuufahamu utumishi wa umma." Bi. Mavika amesisitiza.

Bi. Mavika ameongeza kuwa, mafunzo hayo ni muhimu katika kuendeleza rasilimaliwatu itakayoziwezesha Taasisi za Serikali kufikia malengo ya kuboresha utoaji wa huduma bora kwa ustawi wa taifa.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kupitia Idara ya Uendelezaji Rasilimaliwatu imeandaa mafunzo hayo ya siku mbili kwa Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Wizara.



*Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi akizungumza na Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Wizara wakati akifungua mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Viongozi hao kwenye mabadiliko ya kifikra, kitabia na mtazamo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kiutumishi yaliyofanyika Mtumba katika ukumbi wa Jiji Dodoma.*



*Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa ofisi hiyo mara baada ya kufungua mafunzo kwa Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Wizara (hawapo pichani) yaliyolenga kuwajengea uwezo Viongozi hao kwenye mabadiliko ya kifikra, kitabia na mtazamo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kiutumishi yaliyofanyika Mtumba katika ukumbi wa Jiji Dodoma.*



*Sehemu ya Makatibu Tawala Wasaidizi na Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Sekretarieti za Mikoa na Wizara wakimsikiliza Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Xavier Daudi (hayupo pichani) alipokuwa akifungua mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Viongozi hao kwenye mabadiliko ya kifikra, kitabia na mtazamo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kiutumishi yaliyofanyika Mtumba katika ukumbi wa Jiji Dodoma. Wengine ni Wakurugenzi Wasaidizi kutoka Ofisi ya Rais-UTUMISHI*



7

*Wakurugenzi wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora wakionesha muitikio wao juu ya mafunzo yaliyotolewa Ofisini hapo kwa kununua vitabu vinavyoelezea masuala ya Uongozi*

# KATIBU MKUU MKOMI ASISITIZA DHANA YA URITHISHANAJI MADARAKA KWA WATUMISHI WA UMMA NCHINI

*Na Lusungu Helela - Dodoma*

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi ameitaka Idara ya Uendelezaji Rasilimaliwatu katika Ofisi hiyo kuongeza nguvu katika eneo la mafunzo ya umuhimu wa Urithishanaji wa madaraka kwa Watumishi wa Umma huku akiwataka Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi nchini kuwaandaa watumishi wao ili waweze kuwa viongozi wazuri hapo baadaye.

Amesema Kiongozi mzuri ni yule anayewaandaa watumishi walio chini yake kuwa viongozi wazuri katika siku za usoni huku akionya dhana potofu iliyojengeka kuwa ukiwaandaa watumishi walio chini yako wataichukua nafasi uliyonayo.

Amesema Serikali ina Taasisi nyingi ambazo zinahitaji watumishi hao walioandaliwa vizuri na kwa muda mrefu.

Bw. Mkomi ametoa kauli hiyo Jumatatu Agosti 18, 2025 katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma wakati akizungumza na watumishi wa Ofisi hiyo mara baada ya kutolewa kwa mafunzo ya Uongozi, ikiwa ni muendelezo wa mafunzo hayo ambayo hutolewa kila wiki kwa

hayo ambayo hutolewa kila wiki kwa Watumishi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wao.

Amesema endapo kutakuwa na utamaduni huo wa kurithishana madaraka, watumishi watakaoandaliwa wataenda kuwa viongozi mahali pengine na sio lazima wabaki hapo hapo.

Awali Mwezeshaji wa Mafunzo hayo ya Uongozi, Dkt. Ntangeki Nshala amesema Uongozi sio lazima uwe unawaongoza watu bali ni kuonesha uwezo ulionao katika eneo ulilopo.

Amesema uongozi ni suala binafsi na msukumo uliopo ndani ya mtu ndio maana uongozi unatofautiana katika ya mtu na mtu

Amesema uongozi ni kuonesha njia,kujaribu na kujiamini katika kufanya maamuzi popote ulipo na sio lazima uwe na cheo fulani.

Aidha Dkt. Nshala amesema Watumishi wanahitaji kuwa na ujasiri na ndoto kubwa ya kufanya chochote wanachohitaji huku akionya tabia ya watu wengi ya kushindwa kuonesha uwezo wao kwa kisingizio cha uroho wa madaraka.

Amesema Watumishi waliowengi mara baada ya kuajiriwa husahau kusudi la ndoto zao na hivyo hujikuta wakiishi ili mradi kwa sababu hali zao za kiuchumi huwa zimeimarika kidogo.

"Ukiwa huna ujasiri huwezi kufanya mambo makubwa na hivyo wengi hujikuta wakijidumaza" amesisitiza Dkt. Nshala.

Kufuatia hatua hiyo, Dkt. Nshala amesisitiza watumishi kujitambua na kuwa na dira na maono ya kutaka kuwa nani katika kazi na kwenye jamii kwa ujumla.



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI Bw. Juma Mkomi akikabidhiwa moja ya kitabu cha masuala ya Uongozi kutoka kwa Mwezeshaji wa mafunzo Dkt. Nshala mara baada ya kutoa mafunzo ya Uongozi kwa watumishi wa Ofisi anayoiongoza*



*Wakurugenzi wa Idara na Vitengo katika Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora wakionesha muitikio wao juu ya mafunzo yaliyotolewa Ofisini hapo kwa kununua vitabu vinavyoelezea masuala ya Uongozi vilivyoandikwa na Dkt. Nshala.*


OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA
UMMA NA UTAWALA BORA


MWAKA WA 106
TOLEO NA. 23
GAZETI
LA
DODOMA
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
YALIYOMO


GAZETI


WIKI YA UTUMISHI WA
UMMA 2025
KARIBUNI


DIRA
DHIMA


YA UTUMISHI WA UMMA 2025
KAULIMBIU
MAADHIMISHO YA KITAIFA YA WIKI
e-Wekeza


SISI YA MOYO JAKAYA KIKWETE
TAASISI YA MOYO JAKAYA KIKWETE (JK
MUDA WA KUONA WAGONJWA








HUDUMA KIDIJITI


e-Utendaji
e-Uhamisho
e-Ajira

# 8 KATIBU MKUU MKOMI ATEMBELEA MABANDA YA WIZARA NA TAASISI ZA UMMA KWENYE WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, ATOA SHUKRANI KWA USHIRIKI




*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi (kulia) akimshukuru Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dkt. Maduhu Kazi (kushoto) kwa kutembelea mabanda mbalimbali kwenye Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.*

*Na Mwandishi Wetu - Dodoma*

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi ametembelea mabanda ya Wizara na Taasisi za Umma ili kuona huduma mbalimbali zinazotolewa na ofisi hizo pamoja na kutoa shukrani kwa ushiriki mkubwa katika Maadhimisho hayo ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2025.

"Ninapongeza na kutoa shukrani nyingi kwa Wizara na Taasisi zote za Umma zilizoshiriki katika Maadhimisho haya ya Wiki ya Utumishi wa Umma, zimeonesha ushirikiano mkubwa na idadi ya ushiriki imekuwa kubwa," amesema Bw. Mkomi.

Bw. Mkomi ameseongeza kuwa, kupitia maadhimisho hayo wananchi wanapata fursa ya kuhudumiwa moja kwa moja, kufahamu majukumu ya Wizara na Taasisi pamoja na kupata mrejesho wa utendajikazi kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma.

Aidha, Katibu Mkuu Mkomi ameendelea kutoa wito kwa Watumishi wa Umma, Wananchi na Wadau mbalimbali kuendelea kutembelea katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma ili kupata huduma mbalimbali.



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi (kushoto) akizungumza na Maafisa wa Wizara ya Katiba na Sheria wakati alipotembelea katika banda la ofisi hiyo kwenye Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.*




*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi (kushoto) akisalimiana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko (TPSC), Bw. Shakiru Abdulkarim alipotembelea banda la Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) kwenye Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali Park jijini Dodoma.*

9

# KAMATI YA KITAIFA YA KUDHIBITI VVU, UKIMWI NA MSY MAHALI PA KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA YATAKIWA KUIMARISHA MALENGO YA KUDHIBITI MAGONJWA HAYO

*Na Antonia Mbwambo - Mwanza*

Kamati ya kitaifa ya kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma ambayo inajumuisha Waratibu ngazi ya halmashauri, mkoa na kitaifa, imetakiwa kuimarisha malengo ya kudhibiti magonjwa hayo kwa kuhakikisha Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinasimamia utekelezaji wa Mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY na uwasilishwaji wa taarifa kwa wakati .

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Musa Magufuli kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-UTUMISHI katika ufunguzi wa kikao kazi cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025 ngazi ya Mkoa na Taifa.

Bw. Magufuli amesema, ili kufikia malengo ya kudhibiti magonjwa hayo, mafunzo ya kuwajengea watumishi uwezo wa namna ya kudhibiti yanatakiwa kutolewa na kuteua Kamati za Kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY katika utumishi wa Umma.

Aidha, Bw. Magufuli, amesema kwa kutambua umuhimu wa Afya na Ustawi wa Watumishi wa Umma nchini, Ofisi ya Rais-UTUMISHI iko katika hatua za mwisho za kukamilisha Mwongozo na Waraka kuhusu kudhibiti VVU, UKIMWI na MSY ikiwemo na changamoto za Afya ya Akili mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma.

Bw. Magufuli amewashukuru na kuwapongeza wakuu wa Taasisi za umma nchini kwa kutekeleza kikamilifu afua za kudhibiti VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na kusisitiza kuwa Ofisi ya Rais-UTUMISHI itaendelea kufanya ufuatiliaji kwa lengo la kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji.

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Bw. Balandya Elikana, ametoa rai kwa kila halmashauri kendelea kutekeleza Mwongozo wa VVU, UKIMWI na Magonja Sugu Yasiyoambukiza (MSY) mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma kwa masilahi mapana ya taifa.



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI Bw. Musa Magufuli akitoa hotuba ya Mgeni Rasmi katika kikao kazi cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25*



*Baadhi ya waratibu Kamati ya Mkoa (waliosimama)wakipata picha ya pamoja na mgeni rasmi Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI Bw. Musa Magufuli, baada ya kufungua kikao kazi cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25 Jijini Mwanza, kulia kwake ni Mkurugenzi Msaidizi Anuai za Jamii na Mratibu wa VVU, Ukimwi na Magonjwa Yasiyoambukiza, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Mwanaamani Mtoo na kushoto ni Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza Bw. Balandya Elikana.*



*Mkurugenzi Msaidizi Anuai za Jamii na Mratibu wa VVU, UKIMWI na Magonjwa Yasiyoambukiza, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Mwanaamani Mtoo (kushoto) akifuatilia mada mbalimbali wakati wa kikao kikao kazi cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza.*



*Waratibu wa Kitaifa wakitambulishwa mbele ya Mgeni Rasmi kabla ya kufungua kikao kazi cha kupokea taarifa ya utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa yasiyoambukiza Jijini Mwanza.*

# 10 WATUMISHI OFISI YA RAIS-UTUMISHI WASHIRIKI KONGAMANO LA NNE LA MADEREVA WA SERIKALI WA TANZANIA



*Madereva wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakifuatilia mada mbalimbali wakati wa kongamano la nne la Madereva wa Serikali wa Tanzania lililofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre jijini Dodoma.*

*Madereva kutoka Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Serikali Tanzania Bw. Saidi Kapande kabla ya kuanza kwa kongamano la nne la Madereva wa Serikali wa Tanzania lililofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre jijini Dodoma.*






*Sehemu ya Madereva wa Serikali wakiwa katika kongamano la nne la Madereva wa Serikali wa Tanzania lililofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre jijini Dodoma.*

# 11 WARATIBU WA JINSIA WATAKIWA KUTOA ELIMU KWA WATUMISHI WA UMMA JUU YA NAMNA YA KUKABILIANA NA VIKWAZO MAHALI PA KAZI

*Na Veronica Mwafisi na Antonia Mbwambo - Dodoma*

Waratibu wa Jinsia Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma wametakiwa kutoa elimu kwa watumishi wa umma kupitia Wizara zao juu ya namna ya kukabiliana na vikwazo wanavyokutana navyo katika maeneo yao ya kazi ikiwemo uonevu na dhuluma.

Kauli hiyo imetolewa leo na Mkurugenzi wa Uendelezaji Sera, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Cyrus Kapinga alipokuwa akimwakilisha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI kufungua kikao kazi kilicholenga kupokea taarifa ya utekelezaji wa mipango kazi ya ujumuishwaji wa jinsia ya Mwaka wa fedha 2024/25 jijini Dodoma.

Bw. Kapinga amesema kuna changamoto ya jinsi ya kutoa taarifa kwani taarifa nyingi hazina maudhui ambayo mtu anaweza kupata picha ya ujumuimuishaji wa masuala ya jinsia katika Utumishi wa Umma.

Aidha, Bw. Kapinga amewataka waratibu hao kutumia kikamilifu muda na nafasi waliyopatiwa na waajiri wao katika kuwasilisha utekelezaji wa mpango kazi kwa weledi na ufasaha pamoja na kupokea maoni na ushauri wa namna bora ya utekelezaji kwa Mwaka wa fedha 2025/26.

Kadhalika, Bw. Kapinga ameishukuru Taasisi ya UONGOZI kwa kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu programu za Uongozi kwa Wanawake awamu kwa awamu na kuwezesha kufanyika kwa Semina mbalimbali za mwongozo wa ujumuishwaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma kwa Ngazi ya Wizara.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi Anuai za Jamii na Mratibu wa VVU, Ukimwi na Magonjwa Yasiyoambukiza, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Mwanaamani Mtoo amewaasa Waratibu hao kuhakikisha wanatekeleza miongozo mbalimbali inayohusu ujumuishwaji wa jinsia mahali pa kazi kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa na Serikali.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya UONGOZI, Kaimu Mkuu wa Idara ya Tafiti na Sera, Bi. Carolina Israel amesema, Ofisi ya Rais-UTUMISHI imekuwa ikitoa ushirikiano mkubwa wakati wa mafunzo mbalimbali ya ujumuishwaji wa jinsia mahali pa kazi katika Utumishi wa Umma hivyo, Taasisi ya UONGOZI itaendelea kushirikiana na ofisi hiyo katika kutoa mafunzo hayo kwa ustawi wa maendeleo ya taifa.

Kikao kazi cha Waratibu wa jinsia Mahali pa Kazi katika Utumishi wa Umma kinafanyika kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 01 hadi 02 Septemba, 2025 katika Ukumbi wa Lounge uliopo katika hoteli ya St. Gaspar jijini Dodoma.




WA UMMA NA UTAWALA BORA
DIRA
Kuwa na Utumishi wa Umma
wenye Ufanisi na
Uwajibikaji katika Kufikia
Ustawi wa Taifa.
DHIMA
Institute
Aligning your
organisation


UONGOZI


LEADERSHIP
PROGRAMME
DIRA
Kuwa na Utumishi wa Umma
wenye Ufanisi na
Uwajibikaji katika Kufikia
Ustawi wa Taifa.
DHIMA
Kusimamia Utumishi wa Umma
Institute
Aligning your
organisation

# 12 | UTUMISHI YATWAA UBINGWA WA MPIRA WA MIGUU SHIMIWI KWA MARA NYINGINE

*Na. Eric Amani - Mwanza*

Timu ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Utumishi FC) imefanikiwa kutwaa ubingwa wa mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali (SHIMIWI) kwa upande wa mpira wa miguu, baada ya kuibuka na ushindi mnono wa mikwaju ya penati ambapo Utumishi ilibuka kidedea kwa Penati 4-2 dhidi ya wapinzani wake Tume ua Umwagiliaji katika mchezo wa fainali uliochezwa Septemba 15, 2025 jijini Mwanza.

Ikumbuke Ocktoba 5, 2024 Utumishi FC ilitwaa ubingwa wake kwa mara ya kwanza Mkoani Morogoro ambapo mashindano ya SHIMWI 2024 yalifanyika.

Hii ni mara nyingine tena kwa Utumishi FC kuandika historia ya kuwa miongoni mwa timu zenye mafanikio makubwa zaidi katika mashindano haya, hatua inayodhihirisha ubora, mshikamano na nidhamu ya hali ya juu waliyonayo wachezaji pamoja na benchi la ufundi.

Ushindi huo unaiweka Utumishi kwenye rekodi ya kuwa miongoni mwa timu chache zilizoonesha ubora wa kudumu, kwani ni mara nyingine tena wanatwaa kombe hilo, wakionesha nidhamu ya mchezo, mshikamano na umahiri mkubwa uwanjani.



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa RasilimaliWatu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI Bw. Musa Magufuli (wa sita kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja ya kikosi kizima Ofisi ya Rais - Utumishi jijini Mwanza kwenye kufunga mashindano ya SHIMIWI 2025.*





*Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Bw. Said Mtanda akimkabidhi kombe Nahodha wa timu ya Utumishi baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika mashindano ya SHIMIWI Septemba 16, 2025 jijini Mwanza.*

# 13 TIMU YA MPIRA WA PETE OFISI YA RAIS - UTUMISHI YAFUZU KUINGIA ROBO FAINALI

*Na. Eric Amani - Mwanza*

Timu ya mpira wa pete ya Ofisi ya Rais - UTUMISHI na Utawala Bora imefanikiwa kufuzu kuingia hatua ya robo fainali katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali (SHIMIWI) yanayoendelea jijini Mwanza.

Utumishi imejihakikishia nafasi hiyo baada ya kuibuka na ushindi wa magoli 61 dhidi ya timu ya Mashtaka ambao walipata goli 4 katika mchezo huo wa hatua za Kumi na Sita Bora (Mtoano), jambo lililodhihirisha nidhamu, umoja na maandalizi madhubuti ya kikosi hicho.

Kocha wa timu hiyo, Esther Halla, amepongeza timu yake na akibainisha kuwa matokeo hayo ni ishara ya kujituma na kujiamini kwa timu nzima. Aidha, amewataka wachezaji kuongeza bidii zaidi ili kuhakikisha wanavuka hatua ya robo fainali na kufikia fainali ya mashindano hayo.

Mashindano ya SHIMIWI 2025 yameendelea kuvutia hisia na msisimko mkubwa kutoka kwa mashabiki na watumishi, yakilenga kuimarisha mshikamano, kujenga afya na kuendeleza mshindano ya michezo miongoni mwa Wizara na Taasisi za Serikali.




*Picha ya pamoja Timu ya Mpira wa Pete Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiwa katika mashindano ya SHIMIWI Septemba 8, 2025 jijini Mwanza aidha timu hiyo imefanikiwa kuinga robo fainali katika Mashindano hayo.*




*2.Bi Wema Sarakikya mchezaji wa timu ya mpira wa pete Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akipokea pasi kwa ajili ya kufunga goili, UTUMISHI ilishinda kwa goli 61 - 4 dhidi ya timu ya mpira wa pete ya Mashtaka Septemba 8, 2025 jijini Mwanza.*

# 14 TIMU YA MPIRA WA PETE OFISI YA RAIS - UTUMISHI YAFUZU KUINGIA ROBO FAINALI




*Timu ya riadha ya wanawake Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kuwa mshindi wa kwanza ambapo timu hiyo imefanikiwa kutwaa ubingwa wa mbio za kupokezana (relay) katika mashindano ya SHIMIWI 2025 Septemba 11, 2025 Jijini Mwanza.*

*Na. Eric Amani - Mwanza*

Timu ya riadha ya wanawake ya Ofisi ya Rais - UTUMISHI imeibuka kidedea leo tarehe 11 Septemba, 2025 baada ya kutwaa ubingwa wa mbio za kupokezana (relay) katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yanayoendelea katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Wanariadha wa Utumishi walionesha uwezo mkubwa na mshikamano wa kiufundi uliopelekea kushinda kwa kishindo na kuwapiku wapinzani wao waliokuwa wakipewa nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa huo.

Ushindi huu unaongeza heshima kwa Utumishi, ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika michezo mbalimbali, ikiwa ni kielelezo cha juhudi za kujenga mshikamo na afya bora kwa watumishi wa umma kupitia michezo.

15

# KATIBU MKUU MKOMI APOKEA MAKOMBE YA USHINDI MASHINDANO YA SHIMIWI 2025 ASISITIZA UMUHIMU WA MICHEZO KWA WATUMISHI WA UMMA

*Na Eric Amani na Antonia Mbwambo - Dodoma*

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi, Septemba 24, 2025 amepokea makombe ya ushindi yaliyonyakuliwa na timu ya OfisI yake katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) 2025, yaliyofanyika jijini Mwanza huku akisisitiza umuhimu wa michezo kwa Watumishi wa Umma nchini.

Akizungumza katika hafla fupi iliyofanyika sehemu ya wazi ya Ofisi hiyo, Katibu Mkuu Bw. Mkomi amezipongeza timu zote zilizoshiriki katika mashindano hayo ya SHIMIWI jijini Mwanza kwa juhudi na uzalendo waliouonesha hadi kuibuka mabingwa katika michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu (wanaume) mabingwa nafasi ya kwanza, netiboli (wanawake) nafasi ya tatu, mbio za baiskeli na mchezo wa "darts" walipata ushindi wa nafasi ya tatu wa jumla, aidha kwenye mbio za kupokezana mita 400 (Relay) wanawake waliibuka mshindi wa kwanza na wanaume mshindi wa pili.

Bw. Mkomi amesema ushindi huo ni ishara ya mshikamano, nidhamu na mazoezi ya muda mrefu ya timu nzima. Amesisitiza kuwa michezo si tu burudani, bali pia ni nyenzo muhimu ya kuimarisha afya, mahusiano kazini na kuongeza ufanisi wa kazi.

"Michezo ni afya, hivyo ninawahimiza Watumishi wa Umma msiache kushiriki michezo kwani afya zenu zikiwa nzuri basi huduma zitatolewa kikamilifu kwa wananchi." Amesisitiza na kuongeza kuwa pamoja na kuimarisha afya, pia inaleta ushirikiano.

Amesema Ofisi yake imeweka utaratibu wa watumishi kufanya mazoezi kila siku ya Jumanne na Alhamisi, hivyo amewasisitiza watumishi hao kushiriki kikamilifu.

"Utaratibu wa kufanya mazoezi kila Jumanne na Alhamisi tumeuweka makusudi ili kila mmoja ashiriki, hivyo ukifika muda uliopangwa wa kuanza mazoezi wote tunatakiwa kuelekea kwenye mazoezi," ameongeza.

Pamoja na kuhimiza kushiriki michezo, Katibu Mkuu Mkomi amewataka Watumishi wa Umma kujiepusha na tabia zinazoharibu taswira ya Ofisi. "Haipendezi kuona mtumishi wa umma anafanya mambo ya ajabu huko mtaani, sisi ni kioo, hivyo tunatakiwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuzingatia maadili ndani na nje ya ofisi," amesema.

Naye Mwenyekiti wa michezo wa timu ya UTUMISHI ambaye ni Afisa Tawala Mwandamizi wa Ofisi hiyo, Bw. Charles Shija kwa niaba ya wanamichezo wote, alimshukuru Katibu Mkuu kwa kuwawezesha kushiriki michezo hiyo na kupata ushindi.

Aidha, Bw. Shija pamoja na wanamichezo hao walitumia fursa hiyo kumkabidhi Katibu Mkuu makombe hayo huku wakiahidi kuendelea kujiimarisha zaidi katika michezo kwa ustawi wa taifa.



*Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akifurahia pamoja na Wakurugenzi wa Idara na Vitengo, Watumishi na timu ya michezo ya ofisi hiyo ushindi wa makombe waliyoyapata kwenye mashindano ya michezo ya SHIMIWI.*




*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Juma Mkomi akitoa hotuba fupi kwa watumishi wa Ofisi hiyo katika hafla fupi ya kupokea Makombe ya ushindi wa timu za Ofisi hiyo walioshiriki katika Shirikisho la Michezo ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, (SHIMIWI) lililofanyika jijini Mwanza.*



*Mlezi wa Timu za michezo mbalimbali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi Mwanadawa Nchemwa (watano kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mgeni Rasmi ambaye ni Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Bw. Juma Mkomi (watatu kutoka kushoto) baada ya kukabidhi Kombe la Ushindi uliotokana na mchezo wa netiboli wakati wakati wa mashindano ya SHIMIWI.*



*Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (katikati mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa Idara na Vitengo kutoka katika ofisi hiyo na timu ya washiriki wa michezo ya SHIMIWI mara baada kupokea makombe ya ushindi ya mashindano ya michezo ya SHIMIWI.*



*Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakionyesha makombe ya ushindi kwa Katibu Mkuu wa ofisi hiyo Bw. Juma Mkomi (hayupo pichani) waliyoyapata katika mashindano ya michezo ya SHIMIWI.*

**IMEANDALIWA NA**

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi
wa Umma na Utawala Bora

**Julai 2025**